

WADAU WAKUTANA KUJADILI MIFUMO MBALIMBALI YA KISHERIA INAYOSIMAMIA MASUALA YA USAJILI WA MATUKIO MUHIMU YA BINADAMU NA UKUSANYAJI WA TAKWIMU NCHINI.

HABARI NA PICHA ZA MATUKIO

TAREHE 18 OKTOBA 2016

Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA) kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo Bloomberg's Data for Health Initiative wamekutana hii leo Mjini Bagamoyo Mkoani Pwani kwa lengo la kujadili na kupitia mifumo mbalimbali ya kisheria inayosimamia masuala ya usajili wa matukio muhimu ya binadamu pamoja na kujifunza ili kupata uzoefu kutoka kwa mataifa yanayofanya vizuri katika usajili wa vizazi, vifo na sababu zake, ndoa na talaka pamoja na ukusanyaji wa takwimu za matukio hayo.

Akizungumza na Wadau hao wakati wa ufunguzi wa Mkutano Naibu Katibu Mkuu wa Wizarati ya Katiba na Sheria Bw Amon Mpanju amesema kwa sasa ni wakati muafaka kwa Tanzania kama ilivyo kwa jirani zetu kuipitia upya na kuurejea mfumo wa sheria ili kupata mfumo bora zaidi unaoendana na mazingira na mahitaji ya kipindi hiki ili kusaidia katika utawala, uendeshaji na utunzaji wa kumbukumbu kwa maendeleo ya Taifa na kuutilia mkazo usajili kufanyika mahala popote Nchini, uwe endelevu, na ni walazima na taarifa zake kuwa ni siri kwa lengo la kujenga imani kwa wananchi katika kulinda taarifa hizo zisije kutumika vibaya na kuatarisha usalama wa nchi.

Pia amesisitiza kuwa Serikali inatambua umuhimu wa usajili wa matukio muhimu ya binadamu na tayari hatua kadhaa zimeshachukuliwa ikiwemo kufanya maboresho ya mifumo ya usajili nchini kwa kuanza na utafiti wa kina ambapo mnamo mwaka 2013 kulifanyika tathimini iliyoangalia hali halisi ya mifumo iliyopo na kubaini mapungufu kadhaa yakiwemo mifumo ya kisheria kutokukidhi mahitaji ya sasa na hivyo kuja na mpango wa kitaifa wa Maboresho unaojulikana kama CRVS Strategy ambao utamaliza kabisa changamoto hizo.

Kwa upande wake Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa RITA Bi Emmy Hudson amesema kuwa Sheria na mfumo uliopo sasa wa usajili umepitwa na wakati kutokana na kutokukidhi haja kwani ni wazi kuwa mfumo huo ulirithiwa kutoka serikali za kikoloni tangu mwaka 1917 kwa Serikali ya Mjerumani na baadaye Muingereza ambapo usajili haukuwa ni jambo la lazima na muhimu kwa wenyeji isipokuwa tu kwa Wageni na wale Wananchi wenye asili ya Ki-Asia na hivyo kuchangia hadi leo matukio hayo muhimu ya Binadamu kutokusajiliwa.

Bi Hudson ameongeza kuwa mwisho wa mkutano huo watapata muafaka kwani kuna Wadau mbalimbali kutoka Nchini Ghana na Marekani ambao wamefanya vizuri katika masuala ya usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu na hivyo kupata nafasi ya kuelezea kwa jinsi gani wamefanikiwa ili wadau walioshiriki kutoka Tanzania waweze kujifunza kupitia kwao.

Mkutano huo unaofanyika kwa siku nne umewakutanisha wadau kutoka UNICEF, WHO, Bloomberg, Tume ya kurekebisha Sheria na Wadau wengine wa mambo ya usajili wa matukio muhimu ya Binadamu kutoka Ghana na Marekani.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya katiba na Sheria Bw Amon Mpanju akitoa hotuba ya ufunguzi wa Mkutano wa Wadau kutoka Nchini Ghana, Marekani na mashirika ya Kimataifa ya maendeleo wali-okutana hii leo Mjini Bagamoyo Mkoani Pwani kwa lengo la kujadili Mifumo mbalimbali ya kisheria inayosimamia masuala ya usajili wa matukio muhimu ya Binadamu na Ukusanyaji wa takwimu, kulia kwake ni Kaimu Afisa Mtenjaji Mkuu wa RITA Bi Emmy Hudson na kushoto kwake ni Msajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu kutoka Marekani state ya Hawii Bw Alvin Onaka Mwingine ni Katibu Tawala wa Wilaya hiyo Bi Erica Yegela.



Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu Bi Emmy Hudson akitoa neno la awali la ufunguzi wa Mkutano wa Wadau wa masuala ya usajili wa matukio muhimu katika maisha ya Binadamu uliofanyika Bagamoyo Mkoani Pwani



Washiriki wa Mkutano huo wakiwa katika picha ya pamoja na Mgeni rasmi ambaye ni Naibu katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria Bw Amon Mpanju katika Hoteli ya Stella Maris Mjini Bagamoya Mkoani Pwani.



Washiriki wa Mkutano huo wakifuatilia kwa umakini majadiliano kuhusu maboresho ya mifumo ya sheria zinazosimamia masuala ya usajili wa matukio muhimu ya maisha ya binadamu katika Hoteli ya Stella Maris Mjini Bagamoya Mkoani Pwani.